



**RATIBA YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI
(PRIMARY SCHOOL LEAVING EXAMINATION TIMETABLE)
OKTOBA, 2020**

TAREHE NA SIKU	MUDA (SAA)	NAMBA MFICHO	SOMO
07.10.2020 JUMATANO	2:00 – 3:30	01	KISWAHILI
	3:30 – 4:30		MAPUMZIKO
	4:30 – 6:30	04 04 E	HISABATI MATHEMATICS
	6:30 – 8:30		MAPUMZIKO
	8:30 – 10:00	05 05E	SAYANSI SCIENCE
<hr/> <hr/>			
08.10.2020 ALHAMISI	2:00 – 3:30	02	ENGLISH LANGUAGE
	3:30 – 4:30		MAPUMZIKO
	4:30 – 6:00	03 03E	MAARIFA YA JAMII SOCIAL STUDIES

MAELEKEZO MUHIMU

1. Hakikisha kuwa unayo **Ratiba ya Mtihani ya mwaka 2020** ilioandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.
2. **Kabla ya kufungua bahasha** yoyote yenyewe maswali ya mtihani, hakikisha kwamba **unasoma jina la somo juu ya bahasha husika** na kujihakikishia kuwa somo hilo ndilo linalostahili kufanyika wakati huo kulingana na **Ratiba ya Mtihani**.
3. Endapo utata utajitokeza kati ya **maelekezo yaliyomo ndani ya Karatasi ya Mtihani** na **Ratiba ya Mtihani**, **maelekezo yaliyomo katika karatasi ya Mtihani husika ndiyo yatakayofuatwa**.
4. Watahiniwa **WASIOONA** na wale wenye **UONI HAFIFU** waongezewe **MUDA WA ZIADA WA DAKIKA 10 KWA KILA SAA** kwa Mtihani wa **Kiswahili**, 'English Language', **Maarifa ya Jamii na Sayansi**.
5. Watahiniwa **WASIOONA** na wale wenye **UONI HAFIFU** waongezewe **MUDA WA ZIADA WA DAKIKA 20 KWA KILA SAA** kwa mtihani wa **Hisabati**.
6. Msimamizi wa watahiniwa **WASIOONA** awe Mtaalamu mwaminifu aliye na **uwezo wa kusoma maandishi na alama za 'Braille'**.
7. Watahiniwa wenye **UONI HAFIFU** wapewe karatasi za mtihani na za kujibia zenyewe **maandishi yaliyokuzwa**, zilizoandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania kwa matumizi yao.
8. Karatasi zenyewe majibu ya watahiniwa wenye **UONI HAFIFU** zifungwe kwenye **bahasha za pekee**. Zisichanganywe na karatasi za watahiniwa wenye Uoni wa kawaida.
9. Watahiniwa waelekezwe;
 - (a) Kuingia ndani ya chumba cha Mtihani nusu saa kabla ya muda wa Mtihani na watakaochelewa kwa zaidi ya nusu saa baada ya Mtihani kuanza hawataruhusiwa.
 - (b) Kufuata maelekezo yote yatakayotolewa na wasimamizi wa Mtihani.
 - (c) Kuandika namba ya Mtihani kwa usahihi.
 - (d) Kutofanya mawasiliano ya maneno au kwa njia yoyote baina ya watahiniwa. Ikiwa mtahiniwa ana tatizo anatakiwa kunyoosha mkono ili kuomba msaada kwa msimamizi wa Mtihani.
 - (e) Watakaojihuisha katika udanganyifu watafutiwa matokeo yao ya Mtihani.